**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA**
**MKOA WA MWANZA**

*Unapojibu tangazo hili tafadhali taja*
**Kumb. Na. AB.140/642/01/45** **Tarehe: 04/09/2025.**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA WAKUSANYA MAPATO NAFASI 15

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema anawatangazia Wananchi wote wenye sifa na Vigezo kuomba nafasi za kazi ya Mkataba wa kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

## 1.SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe Raia wa Tanzania
ii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
iii. Awe na Elimu ya Kidato cha nne na kuendelea
iv. Awe na uwezo wa kutumia Kompyuta au Simu janja kwa ufasaha
v. Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
vi. Awe na mdhamini mwenye mali isiyo hamishika yenye thamani ya kuanzia Tshs 10,000,000.00 (milioni kumi) na kuendelea, Dhamana ya mali isiyohamishika itathibitishwa kwa kuwasilisha Halmashauri hati au nyaraka ya umiliki inayotambulika na iliyothibitishwa kisheria kuwa ni mali ya mtoa dhamana.
vii. Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai au kuhukumiwa kifungo Jela katika mahakama yoyote.
viii. Awe tayari kufanya kazi katika Kata yoyote iliyoko ndani ya Halmahauri ya Wilaya ya Sengerema.
ix. Mtu yoyote aliyewahi kufanya kazi na Halmashauri kisha kusababishia hasara ya upotevu wa mapato au kudaiwa na Halmashauri **HARUHUSIWI KUOMBA KAZI YA KUKUSANYA MAPATO**

**2. MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO.**

i. Kukusanya mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo katika eneo la wilaya ya Sengerema kwa kutumia mashine ya kielektroniki (POS).

ii. Kuwasilisha makusanyo yote Benki kupitia akaunti ya mapato ya Halmashauri makusanyo yote yaliyokusanywa ndani ya saa 24 katika siku za kazi au siku ya kwanza ya kazi ya wiki au baada ya Sikukuu.

iii. Kutoa risiti za mashine ya Kielektroniki (POS) kiasi sawa na fedha atakayolipa mlipaji.

iv. Kutunza vifaa vya kukusanya mapato (POS, Rejista) na nyaraka za Benki au Halmashauri zitakazothibitisha uingizaji wa fedha Benki.

v. Kufanya uhakiki kila siku wa makusanyo ya siku na taarifa ya mashine ya kukusanya mapato.

vi. Kuwasilisha Halmashauri mashine ya kukusanyia mapato (POS) kwa ajili ya uchunguzi.

vii. Kufanya kazi nyingine zitakazohusu mapato kadri atakavyoelekezwa na Mwajiri.

**3. MALIPO YA KUKUSANYA MAPATO**

Malipo ya kazi ya ukusanyaji mapato yatakuwa asilimia 5 (5%) ya makusanyo yaliyokusanywa na kuwasilishwa Benki ikijumlishwa na Tshs 60,000.00 kwa kila mwezi.

Maombi yote yatumwe/yaletwe kwa: -

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
S.L.P.175,
**SENGEREMA.**

***Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 18/09/2025 saa 9:30 (saa tisa na nusu Alasiri).***

Tangazo hili limetolewa na: -

Binuru M. Shekidele,
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**SENGEREMA.**

S.L.P 175 SENGEREMA, Phone: +255 (028)2590162, Fax: +255 (028) 2590249
Email:ded@sengeremadc.go.tz,Tovuti: www.sengeremadc.go.tz